https://dspace.org/

# Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi katika Riwaya za S. A. Mohamed, Dunia Yao (2006) na Nyuso na Mwanamke (2010)

**Muigai, Mary Njambi; Mwamzandi, Issa; Oduori, Robert**

**2024**
Journal of Kiswahili and Other African Languages
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/867
Muigai, M. N., Mwamzandi, I., & Oduori, R. (2024). Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi katika Riwaya za SA Mohamed, Dunia Yao (2006) na Nyuso na Mwanamke (2010). Journal of Kiswahili and Other African Languages, 2(1), 10-19.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 1 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i1.409


# Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi katika Riwaya za S. A. Mohamed, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso na Mwanamke* (2010)

**[1]Mary Njambi Muigai, [2]Issa Mwamzandi & [1]Robert Oduori**
*[1]Chuo Kikuu cha Moi*
*[2]Chuo Kikuu cha Kabianga*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-12-02*
*Rekebishwa: 2024-01-13*
*Kubalika: 2024-01-26*
*Chapishwa: 2024-01-27*

***Maneno Muhimu***
Simulizi kuu
Uanuwai
Ubaadausasa
Uchopekaji

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Muigai, M. N., Mwamzandi, I. & Oduori, R. (2024). Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi katika Riwaya za S. A. Mohamed, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso na Mwanamke* (2010). *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 2(1), 10-19.

*Copyright © 2024 The Author*
CC BY

**Ikisiri**
Makala haya yanachunguza matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi katika riwaya mbili za S. A. Mohamed, *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Ubaadausasa ambayo hupendekeza uanuwai wa mawazo kwa kukaidi kuwepo na mtazamo mmoja wa kueleza ulimwengu na tajriba za binadamu, au simulizi kuu. Uchanganuzi umedhihirisha kuwa mwandishi wa riwaya hizi alitumia kimakusudi vipengele vya kibaadausasa ili kukaidi simulizi kuu zilizotawala. Riwaya hizi zilitumia uchopekaji wa vipande vya simulizi kuvuruga urazini, mshikamano, na muumano wa usimulizi wa riwaya za kimapokeo. Kimaudhui, riwaya hizi zinasaili mwelekeo chanya uliohusishwa na uhuru. Zinaonyesha kuwa mataifa mengi ya Afrika yametawaliwa na hali ya utamauishi baada ya uhuru. Vilevile, misaada inayotolewa na mataifa ya ulaya hutumika kama chambo cha kueneza ukoloni mamboleo katika mataifa ya Afrika. Hali kadhalika, riwaya hizi zinaonyesha changamoto ambazo wahamiaji hupitia wanapohamia ughaibuni kutafuta maisha bora. Ni bayana kuwa mwandishi wa riwaya hizi ametumia mtindo wa uandishi wa ubaadausasa kama mbinu ya kiumbuji inayokaidi uandishi wa kimapokeo. Vilevile, riwaya hizi zimetumika kudhihirisha fujo, ghasia, na ukosefu wa mshikamano katika ulimwengu wa karne ya ishirini na moja.

## Utangulizi

Riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika miaka ya hivi karibuni zinakaidi uandishi uliozoeleka wa kimapokeo uliopendekezwa na akina Aristotle, na kugeukia mtindo mpya wa uandishi wa kimajaribio wa kibaadausasa. Katika fasihi ya Kiswahili, mtindo huu umeanza kutumika katika mwongo wa mwisho wa Karne ya Ishirini kama njia ya kuonyesha mabadiliko yanayotokea katika dunia ya sasa hasa kutokana na utandawazi (Mohamed, 2002). Kuzuka kwa mtindo huu wa uandishi kumeleta mabadiliko makubwa katika riwaya ya Kiswahili kwa kukiuka kaida ya uandishi wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Badala yake riwaya hizi ni changamano katika kiwango cha msuko kupitia matumizi ya uchopekaji wa vipande vya simulizi. Riwaya hizi hazina mshikamano na muumano wa hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Badala yake, vipengele katika hadithi vimechupwa huku na kule na kuunda vipande vidogo vidogo vya hadithi au visa ambavyo hutumika kama malighafi ya kuunga simulizi hizo. Matukio nayo yanaonekana kama vipengele vinavyojitenga na vingine badala ya vipengele hivi kuingiliana, kujengana, na kukamilishana (Bertoncini, 2009;

Mwamzandi, 2013). Kwa hali hiyo, imebainika kuwa riwaya hizi zinaenda kinyume na riwaya za kimapokeo zilizojikita katika uhalisia na badala yake kutumia uchopekaji wa vipande vya simulizi kudhihirisha upya katika riwaya ya Kiswahili ilioandikwa kwa mtindo wa kimajaribio wa ubaadausasa.

Waandishi mbalimbali (Lewis, 2001; Mohamed, 2002; Wamitila, 2003 na Bertoncini, 2009) wanakubaliana kuwa simulizi tofauti katika kazi za kibaadausasa zimetumiwa kuyashughulikia masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kiteknolojia kwa namna ambayo uhalisia haungeweza kuyazungumzia. Riwaya za S.A. Mohamed, *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* ni kielelezo cha kazi zinazoshughulikia masuala nyeti yanayoathiri mataifa ya Afrika. Kama wanavyokubaliana wataalam mbalimbali (Magaju, 2004; Bakari, 2008; Mwamzandi, 2013) mtindo uliotumika katika riwaya hizi, umezifanya kuwa ngumu kusomeka na kueleweka. Kwa hiyo, huenda ukaitenga hadhira hasa isiyobobea katika fani mamboleo za kifasihi. Kwa kutumia Nadharia ya Ubaadausasa, makala haya yamezibainisha simulizi zilizochopekwa ndani ya riwaya hizi kuwa simulizi kuu. Simulizi hizo ni pamoja na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika, na suala la uhamiaji wa waafrika katika mataifa ya ulaya.

## Misingi ya Kinadharia

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ubaadausasa inayohusishwa zaidi na mwanafalsafa, Jean Francois Lyotard (1979). Katika makala yake maarufu, *The Post-Modern Condition: A Report on Knowledge* Lyotard anaueleza ubaadausasa kama hali ya kutilia shaka na kuzipinga simulizi kuu mbalimbali. Anatumia neno simulizi kuu kurejelea nadharia na mifumo jumuishi inayodai kumiliki ukweli halisi, au kutoa maelezo jumuishi ya namna tunavyopaswa kuutazama ulimwengu, au kutoa suluhisho la matatizo yote ya binadamu. Simulizi kuu halisi ambazo Lyotard anazipinga ni mfumo wa Umarx, mwondoko wa Usasa na mradi wa Mwamko wa Kitaaluma. Anasema kuwa mifumo hii haikuweza kutimiza malengo ambayo iliahidi. Umarx, kwa mfano, ulisisitiza kuleta ukombozi wa binadamu kutokana na minyororo ya ubepari. Hata hivyo, haukuweza kuleta uhuru na ukombozi ulioahidi, hivyo basi hauwezi kuaminiwa tena. Kwa mujibu wa Lyotard, simulizi kuu kama hizi hazipaswi kutiliwa maanani.

Lyotard na wanaubaadausasa kwa jumla wanashikilia wazo kuwa hakuna ukweli halisi (Sim, 2001; Barry, 2002). Wanakataa kuamini kwamba kuna misingi isiyopingika au taratibu maalumu za kutenda jambo. Wanazipinga simulizi kuu zinazodai kuhodhi ukweli halisi usioweza kupingika, au kudai kuleta mabadiliko na maendeleo katika kila hatua ya uhai wa binadamu. Simulizi hizo ni kama vile umuundo, elimu, dini, na utamaduni (Sim, 2001; Barry, 2002; Rivkin & Ryan, 2004). Katika makala haya neno simulizi kuu limetumika kurejelea aina yoyote ya hadithi au simulizi iliyozoeleka na kuaminiwa kuwa ya kweli. Makala haya yametumia mhimili huu kuzihakiki simulizi kadhaa kama vile simulizi kuhusu uhuru wa Mwafrika, ajenda za mataifa ya ulaya barani Afrika na hatimaye simulizi kuhusu uhamiaji wa Waafrika katika mataifa ya Ulaya. Kwa kuwa wanabaadausasa huzisaili simulizi kuu, Lyotard (1979) anapendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo. Anaeleza simulizi ndogo kama vikundi vya muda vya watu vinavyopaswa kurekebisha ukandamizaji unaoenezwa na simulizi kuu. Makala haya yamechukulia simulizi ndogo kama njia mbadala za kupambana na hali tofauti za maisha. Katika makala haya, mtindo wa uandishi wa ubaadausasa umejitokeza kama njia mbadala ya kuuelezea ulimwengu wa sasa kwa njia ambayo, kama anavyosema Khamis (2005, 2008), uhalisia haukuweza kueleza.

Mhimili mwingine muhimu unaohusishwa na Lyotard (1979) na wanaubaadausasa kwa jumla ni kuwa ulimwengu hauna mshikamano. Badala yake kuna njia tofauti na anuwai za kuutazama ulimwengu (Deleuze & Guattari, 1980). Lyotard anazua dhana ya 'utofauti' kupinga mifumo yoyote ambayo huleta hali ya kujumuisha *(homogenization)* tajriba tofauti za binadamu. Badala yake anapendekeza mifumo inayozingatia tofauti anuwai zilizoko. Kwake Lyotard, kutokubali kuwepo kwa tajriba tofauti kunaleta dhana ya ukandamizaji ambao anaukataa. Anasema kuwa hakuna sheria jumuishi inayofaa kuongoza mawazo yetu. Kama wanavyosema Deleuze na Guattari (1984), wanaubaadausasa wanajali na kusherehekea 'utofauti' na 'uanuwai' katika tajriba tofauti za binadamu wala si mshikamano. Katika riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* wazo hili la 'utofauti' limedhihirika kupitia uandishi mpya wa kibaadausasa ambao ni tofauti na riwaya za kimapokeo. Riwaya hizi zinakaidi uandishi wa kimapokeo uliokuwa na muumano na mshikamano wa hadithi na matukio kutoka mwanzo hadi mwisho. Badala yake riwaya hizi zina vipengele vidogo vidogo vya simulizi vilivyochopekwa huku na kule, dhana ambayo katika makala haya, tumeiita uchopekaji wa vipande vya simulizi.

**Mbinu za Utafiti**
Makala haya yametumia mkabala wa utafiti kiustahilifu kukusanya na kuhakiki data. Usampuli wa kimaksudi ulitumiwa kuteua riwaya za S.A. Mohamed zilizoandikwa katika mwongo wa kwanza wa karne ya ishirini na moja. Riwaya hizi zilidhihirisha upya kwa kukaidi mtindo wa kimapokeo uliojikita katika uhalisia. Upitiaji wa machapisho mbalimbali kutoka kwa mtandao, majarida, na vitabu ulifanyika maktabani ili kufanikisha malengo ya makala haya. Data ilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa riwaya zilizoteuliwa. Vipengele vya kibaadausasa vilivyojitokeza kwa wingi katika riwaya zote mbili viliteuliwa kwa mbinu ya kimaksudi na kunakiliwa kwa daftari. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Ubaadausasa. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kupitia maelezo ya kinathari.

**Uchopekaji wa Vipande vya Simulizi katika *Dunia Yao (DY)* na *Nyuso za Mwanamke (NZM)*[1]**
Wataalamu mbalimbali (Best & Keller, 1991; Sim, 2001; Khamis 2008; Mwamzandi, 2013) wanakubaliana kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mtindo mamboleo unaokiuka kaida za awali za uandishi wa kimapokeo uliokuwa na muundo wenye muumano na mshikamano. Kama anavyosema Khamis (2003) matumizi ya vipande vidogo vya hadithi visivyounganika vizuri ni mbinu ya kimakusudi anayoitumia mwandishi kama dhihirisho la ukosefu wa mshikamano katika jamii ya kisasa barani Afrika. Riwaya za *DY* na *NZM* kama mojawapo ya riwaya za Kiswahili zilizotumia mbinu ya uchopekaji wa simulizi zimedhihirisha ukweli huu kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata:

> Katika simulizi na mapito yake, vipandevipande – si lazima vishikane. Unavimwaga tu vipande vyenyewe kama unaatika mbegu kwenye shamba la Sanaa. Unafanya hivyo kuwaacha wasomaji waunge wenyewe vipande vya maana zao, huku maneno mengine ukiyajengea vivuli ili kuwatenga makusudi watafute maana zao badala ya kuzipata maana kibungabunga…kipande hapa… kipande pale. Vipande vya

[1]Kuanzia sehemu hii, mijadala katika makala haya yametumia vifupusho *DY* na *NZM* kurejelea riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* mtawalia.

> 'allegory'. Vipandevipande vya ngano mpya. Ngano ya tafrani-za-kileo katika usogori mpya (*DY* uk. 9, 68).

Katika dondoo tumeelezwa kuwa simulizi katika kazi ya fasihi hujikita katika 'tafrani-za-kileo' (*DY* uk. 68). Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018) tafrani ni fujo, ghasia au hali ya kutokuwa na utulivu. Kwa hivyo, simulizi za tafrani za kileo ni simulizi zinazozungumzia fujo, ghasia na ukosefu wa mshikamano katika ulimwengu wa sasa. Aidha, tumelezwa kwenye dondoo kuwa ni jukumu la msomaji kuunga vipandevipande hivyo vya hadithi ili kuwasilisha maana zao wenyewe. Haya ni kweli katika riwaya tulizoshughulikia katika makala haya kwa sababu maudhui yanayopatikana yamechopekwa huku na huku bila mpangilio maalumu. Ni jukumu la msomaji au mtafiti kuyakusanya na kuyaunganisha pamoja ili yaweze kuelezeka.

Uchopekaji wa vipande vya simulizi katika *DY* na *NZM* umejitokeza kupitia matumizi ya visa na vijihadithi vingi visivyokuwa na muumano au mshikamano. Kwa kuwa visa hivyo ni vingi, makala haya yameteua simulizi tatu pekee. Simulizi ya kwanza inahusiana na maana ya uhuru katika mataifa ya Afrika baada ya uhuru. Simulizi ya pili nayo imejadili ajenda za mataifa ya Ulaya barani Afrika, na mbinu zinazotumiwa kuziendeleza ajenda hizo. Hatimaye, tumejadili simulizi inayohusiana na uhamiaji katika mataifa ya Ulaya na athari zake. Simulizi hizi zimeteuliwa kimakusudi kwa kuwa zimejitokeza kama aina ya simulizi kuu. Tumezihakiki simulizi hizo kwa mujibu wa Nadharia ya Ubaadausasa kama ilivyofafanuliwa na Lyotard (1979).

**Uhakiki wa Simulizi kuhusu Maana ya Uhuru wa Mwafrika**

Ukoloni ulihusishwa na utumwa na unyanyasaji kwa Mwafrika (Ndege, 2009), mambo yanayodhihirisha ukosefu wa haki na usawa. Hali ya kutaka kujitoa katika utumwa wa Wakoloni na kuleta haki na usawa ni baadhi ya mambo yaliyochochea Waafrika kutaka kupigania uhuru. Katika muktadha wa ubaadausasa, uhuru wa Mwafrika kutoka kwa mkoloni basi unaweza kuchukuliwa kama aina ya simulizi kuu. Hii ni kwa sababu uhuru ungewawezesha Waafrika kujitawala kisiasa na kuwakomboa kutoka unyanyasaji wa mkoloni. Hata hivyo, riwaya ya *NZM* inadhihirisha kuwa mambo yaliyoahidiwa na uhuru kama vile haki, usawa, maendeleo, na nafasi za kazi hayakutimia. Nikimnukuu mwandishi anasema:

> Wanabaki kujiuliza kinatokea nini katika maisha yao? Laana ya Mungu au mapuuza ya binadamu mwenyewe? Ya wapi yale waliyoelezwa kuhusu usawa? Ya wapi yale waliyoahidiwa? Uhuru na kazi. Uhuru na haki. Uhuru na maendeleo. Uhuru na nini sijui… Yako wapi matunda waliyoambiwa watagawiwa akishaondoka Mzungu na Mwarabu? (*NZM* uk. 37).

Kutokana na dondoo ni bayana kuwa wananchi hawafurahii matunda ya uhuru kama yalivyoahidiwa. Riwaya za *NZM* na *DY* zinadhihirisha kwa kina kuwa badala ya raia kufurahia matunda ya uhuru kuna dhuluma, kero, na unyanyasaji wa kila aina. Viongozi kama vile Bwana Hila wanahusika katika unyakuzi wa ardhi ya wanyonge na kujitenga mbali na raia waliomchagua (*NZM* uk 35, 37). Aidha, mipaka kati ya matajiri na maskini inaendelea kupanuka. Kwa mfano, maskini wanaishi katika vibanda vilivyojengwa kwa majamvi mabovu, masalia ya madebe yaliyochoka na mbao zilizomung'unyuliwa na mchwa miongoni mwa vifaa vingine duni. Matajiri nao wanajenga

majengo ya kifahari yanayopendeza aina ya *Villa*[2] (*DY* uk. 31, 32, 65). Hili ni dhihirisho la ukosefu wa usawa ulioahidiwa na uhuru.

Aidha, kuna ukosefu wa maendeleo baada ya uhuru. Kwa mfano, katika *DY* Ndi- analalamika kuwa katika miaka arobaini na miwili ya uhuru taifa linakwenda 'gizani kuliko kweupe' (uk. 2, 5). Kauli hii inaashiria kuwa taifa halijapata maendeleo yoyote baada ya uhuru na badala yake linarudi nyuma. Hali sawia na hii inajitokeza katika *NZM* ambapo Faisal anaonyesha hali ya kutamausha kutokana na kuzoroteka kwa maisha nchini Tanzania baada ya miaka 37 tangu atoke huku na kwenda Arabuni (uk 8, 12). Anasema kuwa nafuu iliyotarajiwa kuletwa na uhuru haipo tena. Badala yake mji umejaa uchapwa, uchafu, hatari, fujo, na ukatili. Kuna uchafuzi wa mazingira; vinyesi, takataka, na mifuko ya plastiki imetapakaa kila mahali. Makaro yanabwabwaja maji machafu na vitalu havina miti wala maua. Zamani vitalu vilijaa miti iliyofunua urembo wa maua juu ya vigoo (*DY* uk. 31-35; *NZM* uk 8-13). Vilevile, kuna miundo misingi duni. Kwa mfano, barabara ni za mchanga na zimejaa mashimo kwa kuwa hazijawekwa lami. Nyumba nazo ni vibanda dhaifu vya matope ambavyo kavijapakwa rangi au chokaa tangu vijengwe (*DY* uk. 35-36; *NZM* uk. 12-14).

Mbali na kuwa na majengo duni, vituo vya afya ni duni na havitoi huduma bora kwa raia wake. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa hospitali ni kama mabanda na hazina dawa. Madaktari nao ni wachache (*DY* uk. 41-42). Fauka ya hayo, kuna ukosefu wa usalama ambapo watu wanaiba, kunyang'anya, na kuuana ovyo ovyo (*DY* uk. 32). Aidha, kuna ukosefu wa ajira na nafasi chache za kazi zinazopatikana hutolewa kwa njia ya mapendeleo kutegemea unayemjua wala sio kutegemea elimu, akili, na busara. Zaidi, nafasi hizo zinatolewa kwa wale ambao wanaoitika 'ndiyo' kila wakati" (*DY* uk. 16); yaani, wale ambao hawawezi kupinga sera na tabia mbovu za wakubwa wao. Wafanyikazi waadilifu kama Ndi- wanaodhubutu kuwapinga wakubwa wao kwa sababu ya visa vya ufisadi na ubadhirifu wanafutwa kazi *(DY* uk. 17, 81, 188). Katika muktadha wa ubaadausasa, uhuru wa Mwafrika ni aina ya simulizi kuu ambayo haiwezi kuaminiwa tena. Haukuweza kuleta haki, usawa, maendeleo, na kubuni nafasi za kazi kama ulivyoahidi. Badala yake tunapata kuwa raia wanaendelea kunyanyaswa na viongozi waliowachagua.

**Uhakiki wa Ajenda za Mataifa ya Ulaya Barani Afrika**

Mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu, hususan mataifa ya Afrika, yako nyuma kimaendeleo yakilinganishwa na yale ya mataifa ya Magharibi. Kwa mtazamo wa nje, mataifa ya Ulaya pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali huonekana kuyajali mataifa ya Afrika na aghalabu hutoa misaada ili "kuyainua" na "kuyaondoa" katika lindi la umaskini. Lakini, uchunguzi wa kina katika riwaya za makala haya unadhihirisha kuwa hali ni tofauti. Mataifa ya Ulaya hulenga kuendeleza ajenda zao wenyewe kwa njia iliyofichika, wala sio kuendeleza ajenda za mataifa ya Afrika. Kama anavyosema Sim (2013), wanaubaadausasa hulenga kufichua itikadi za kilaghai zilizofichika katika mifumo mbalimbali, iwe ya kijamii, kiuchumi, na kidini. Katika dondoo linalofuata ni dhahiri kuwa mojawapo ya ajenda za mataifa ya Ulaya ni kuyatawala na kuyadhibiti mataifa ya Afrika:

> "Sisi ndio tuliopewa haki ya kuudhibiti ulimwengu." Nikawahi kumsikia Mzungu mmoja aliyekuwa akibwabwaja kwa jeuri alipokwishaikata chupa ya Gorbachev. "Tulipoona haitoshi Ulaya na mabara ya Mungu matupu duniani na watu

[2] *Villa* ni nyumba kubwa ya kisasa iliyozungukwa na bustani. Aghalabu, hukodishwa kwa watu walio likizoni (Hornby 2020).

> wasiofahamu faida ya ardhi kama nyinyi mmeikalia kivivu, tulikuja kuing'wapura!" Waswahili wote walicheka na kupandisha gilasi zao za Gorbachev. "Ndiyo… Ndiyo…aliendelea yule mzungu. "Akili zetu ndizo zilizotupa haki tutawale. Nguvu na ubora wetu wa kimaumbile ndio uliotuwezesha kujitawala. Inafaa mshukuru kukufanyieni mengi katika kujifanyia sisi wenyewe. Sasa mwangaza umezagaa Afrika." Waliokuwepo wote walicheka kwa mzaha huo. Wageni kwa wenyeji (*DY* uk. 126).

Neno 'sisi', katika dondoo linatumiwa na Mzungu kurejelea mataifa ya Ulaya huku neno 'Waswahili' likitumiwa kuwarejelea watu wa mataifa ya Afrika. Mzungu anahalalisha ukoloni mkongwe dhidi ya mataifa ya Afrika. Anaeneza kasumba kuwa Waafrika ni watu duni na wasiojielewa, huku ikiwatukuza Wazungu kama watu wenye akili iliyopevuka. Uenezaji wa kasumba hii dhidi ya Waafrika basi ni mbinu mojawapo wanayoitumia Wazungu kutawala mataifa ya Afrika kisiasa. Inavyobainika katika dondoo ni kuwa Wazungu wamefaulu kuieneza kasumba hii. Hii ni kwa sababu maneno ya Mzungu hayajawakera Waafrika kwa njia yoyote. Wanacheka tu na kushangilia. Riwaya ya *DY* inafichua ajenda hasi ya kasumba hii na kujaribu kuwazindua Waafrika kuwa binadamu wote ni sawa. Hata hivyo, mazingira ambamo kila mmoja amezaliwa na kulelewa huweza kuathiri namna anavyofikiri na kutenda (*DY* uk. 45, 47, 172-173).

Aidha, kasumba hiyo inatumika kuyadhibiti na kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi. Wazungu wanapuuzilia mbali bidhaa zilizotengenezewa ndani ya Afrika. Wanawarai Waafrika kuacha kununua bidhaa za Dar es Salam (Jiji mashuhuri la nchini Tanzania) wakiwalaghai wanunue bidhaa kutoka majiji ya mataifa ya nje kama vile; London (Uingereza), Paris (Ufaransa), New York (Marekani) na kwingineko (*NZM* uk. 194). Kasumba hii imewawezesha wazungu kupata soko la bidhaa zao katika mataifa ya Afrika.

Misaada inayotolewa na mataifa ya Ulaya hutumika kama chambo cha kuchochea utiifu kwa mataifa ya Afrika. Baada ya kuipokea, mataifa ya Afrika hayana budi kufuata amri na sheria kutoka kwa mataifa ya Ulaya. Tunaelezwa kuhusu Marekani ambayo imerejelewa kwa jina 'Supreboymmoja' ambayo ni mfano wa sarafu yenye pande mbili. Kwa mkono mmoja imeshika 'haki, uadilifu, huruma, na ruzuku'. Kwa upande mwingine kuna uharibifu na maangamizi (*DY* uk. 45-46). Mkono wa haki, uadilifu, huruma, na ruzuku hudhihirika kupitia utoaji wa misaada kwa mataifa ya Afrika. Baadhi ya misaada hii inatolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali kama *Umoja wa Akina Mama.* Shirika hili linafadhili miradi mbalimbali kwa wanawake kama vile: kupika uji na maandazi, kusuka mikoba na vikapu, na kulima mihogo, viazi na ndizi (*NZM* uk. 190-191). Hata hivyo, miradi hii ni duni na haiwezi kuchangia katika maendeleo ya taifa. Kama anavyosema Nana, miradi hii inalenga kuididimiza Afrika katika lindi la umaskini na utegemezi.

Aidha, kuna misaada ya silaha. Kwa mtazamo wa nje misaada ya silaha hulenga kukomesha vita katika mataifa ya Afrika. Kinaya ni kuwa silaha hizi zinatumika kuchochea vita katika mataifa ya haya. Mataifa ya Ulaya yanapate nafasi ya kunyakua almasi na rasilimali nyinginezo zinazopatikana barani Afrika (*DY* uk. 46, 48). Aidha, kuna misaada ya kondomu inayotolewa na hata kufanyiwa matangazo kemkem kwenye vyombo vya habari (*NZM* uk. 181). Licha ya kuwa mipira hii inalenga kuzuia uenezaji wa ugonjwa wa ukimwi, kuna uwezekano kuwa mipira hii hatimaye itauziwa. Mataifa ya Afrika hayatakuwa na budi kuinunua kwa sababu tayari watu watakuwa wamezoea kuitumia. Hii ni njia ya mataifa ya ulaya ya kutafuta soko la bidhaa zao. Vilevile, inaweza kuchukuliwa kama njia ya kufanyia ugonjwa huu utafiti zaidi. Waafrika basi wanatumika kama

maabara ya kufanyia utafiti magonjwa yanayozuka kwa kuwa mataifa ya Ulaya hayajali kama wataishi au wataangamia. Matangazo haya ya kuhimiza ngono pamoja na matangazo yanayopendekeza fesheni za mavazi ya kisasa ya *tumbo-cut*[3] na muziki wa *rap*[4] (*NZM* uk. 181) yanalenga kuuchujua utamaduni wa Kiafrika uliojikita katika maadili.

Upande wa maangamizi unadhihirika wakati mataifa ya kigeni hususani, Marekani, hutoa amri na kuwekea watu wa mataifa ya Afrika masharti mbalimbali ambayo wanafaa kuyafuata. Wanaokosa kutii wanawekewa vikwazo mbalimbali hasa vya kiuchumi kama njia ya kuwaadhibu (*DY* uk. 45-46). Mataifa ya ulimwengu wa tatu hayana budi kufuata amri zinazotolewa kwa sababu, kwanza hayana uwezo wa kuzipinga 'nguvu za kiungu' za *Superboymmoja*[5]. Yakithubutu yanaweza kuangamizwa. Pili, mataifa haya yana mahitaji mbalimbali yawe ya pesa, misaada na mikopo ambayo yanategemea *Superboymmoja* ayasaidie (*DY* uk. 45-46). Uhitaji katika mataifa ya ulimwengu wa tatu unayafanya mataifa haya kunyenyekea chini ya huyu "Superboymmoja" ili kupata usaidizi yanaouhitaji kutoka kwake. Ajenda kuu ya kuweka vikwazo hivi ni kuyawezesha mataifa ya Ulaya kuyatawala mataifa ya Afrika Kiuchumi. Kwa mfano, yanawashurutisha Waafrika kuwauzia kampuni na viwanda vyao vya mafuta, forodha na kampuni na maji na umeme kupitia sheria wanazozitunga wenyewe (*NZM* uk. 193)**.** Hii ni mbinu iliyofichika inayotumiwa na mataifa ya Ulaya kuwekeza katika mataifa ya Afrika na kuendelea kujitajirisha huku ikiwapunja wenyeji. Aidha, mataifa ya Afrika yanalazimika kutumia fedha kugharamia ujuzi wa kiteknolojia unaotoka katika mataifa ya Ulaya. Haya yanayawezesha mataifa ya ulaya kuendelea kuyatawala mataifa ya Afrika kiuchumi. Hatimaye, mataifa ya Ulaya yanaweza kuyatawala na kuyadhibiti mataifa ya Afrika katika kila sekta ya maisha; uchumi, afya, elimu, na kadhalika (*DY* uk. 43-47). Mwafrika anabaki kuwa mpokezi tu na mfuasi wa mambo yote kutoka mataifa ya Ulaya yenye nguvu.

**Uhakiki wa Simulizi inayohusu Uhamiaji wa Waafrika katika Mataifa ya Ulaya**

Sehemu hii imejadili simulizi inayohusiana na uhamiaji ambapo Waafrika hutoka nchi zao na kuhamia mataifa ya Uaya, hususani Uingereza. Simulizi kuu inayohusishwa na swala nzima la uhamiaji ni kuwa maisha katika mataifa ya Ulaya ni bora yakilinganishwa na maisha katika mataifa ya Afrika. Riwaya ya *DY* inadhihirisha kuwa Waafrika huhamia Uingereza ili waweze kuyaboresha maisha yao. Hufanya hivyo ili kuepuka changamoto zinazopatikana katika mataifa yao. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa usalama (*DY* uk. 123) na ukosefu wa kazi (*DY* uk. 117). Aidha, nafasi chache za kazi zinazopatikana Afrika hutolewa kwa upendeleo (*DY* uk. 16, 115). Vijana waliosoma kama Mtima wanatamauka na kuzembea tu mabarazani. Wengine kama Yungi wanaingilia ukahaba ili kujikimu kimaisha (*DY* uk. 117, 150, 151). Elimu iliyochukuliwa kama ufunguo wa heri katika enzi za akina Ndi- (uk 15) inaishia kuwa simulizi kuu. Haiwezi kutegemewa tena na vijana katika mataifa ya Afrika katika karne ya ishirini na moja. Kwa mfano, Ndi- anasema kuwa elimu imekuwa 'upuuzi mtupu… Kusoma na kutosoma ni sawa'. Hii inaonyesha kuwa vijana wote, wenye elimu na wasio nayo, wanahangaika kutokana na ukosefu wa kazi. Wengi wanaamua kuhamia mataifa ya Ulaya kwa lengo la kuyaboresha maisha yao. Katika *DY* tunaelezwa kuwa viza ya kuingia Uingereza inalinganishwa na 'donge la dhahabu na ufunguo wa peponi' (*DY* uk. 123). Ni dhahiri kuwa kupata

[3] *Tumbo-cut* ni mtindo wa kisasa wa kuvaa kishati kinachoning'inia tumboni na kuacha nafasi wazi kabla haijaja suruali au sketi kiunoni (Mohamed 2006).
[4] *Rap* ni mziki wa kisasa ambapo mwimbaji huzungumza kwa kufuata mdundo maalum wa kimziki wenye urari wa maneno au sauti (Hornby 2000).
[5] *Superboymmoja* ni neno alilounda mwandishi kurejelea nchi ya Marekani (Mohamed 2006).

viza ya kuingia Uingereza ni jambo la thamani sana kwa kuwa hudhaniwa itawawezesha wahamiaji kupata raha na furaha. Uingereza kwenyewe kunalinganishwa na '*The Promised Land*' yaani 'Nchi ya Ahadi' (*DY* uk. 112). Dhana hiyo inaashiria fahawati kuwa Uingereza ni mahali pazuri pasipo na changamoto zozote. Riwaya ya *DY* inalenga kuisali simulizi kuu hii kwa kubainisha changamoto mbalimbali ambazo wahamiaji hupitia. Riwaya hii inadhihirisha kuwa simulizi kuu hii, kama zilivyo simulizi kuu nyingine, haiwezi kuaminiwa tena katika kuwaletea Waafrika afueni. Hii ni kwa sababu suala nzima la uhamiaji hukumbwa na matatizo si haba kuanzia matayarisho ya usafiri, safari yenyewe, na maisha katika mataifa ya Ulaya.

Mojawapo ya changamoto ambazo wahamiaji hupitia linahusiana na mahitaji ya kifedha. Katika maandalizi, mhamiaji huhitaji fedha za kuwalipa wanaomsaidia kutafuta stakabadhi za usafiri, pamoja na kumpa ushauri unaohusiana na safari yenyewe. Kwa mfano, Mtima analazimika kumlipa wakala anayemtayarishia safari dola za kimarekani elfu mia nne kabla ya maandalizi ya safari (*DY* uk. 123, 80). Hii ilikuwa akiba yake yote aliyokuwa nayo. Vilevile, kuna fedha za kuonyesha ubalozi kuwa unaweza kujikimu unapofika Uingereza. Mtima anaazimwa fedha hizi na shoga yake, dola elfu tano (*DY* uk. 123). Isitoshe, mhamiaji huhitaji fedha zaidi za kumlipa wakili atakayebuni kisa kinachoeleza sababu za kutaka kuihama nchi yake na kwenda Uingereza. Mchakato huu wa kubuni kisa huandamana na ulaghai mwingi ambapo mkimbizi hulazimika kubadilisha uraia wake ili uafiki maelezo yaliyotolewa katika kesi yenyewe. Mtima, kwa mfano, analazima kuubadilisha uraia na kuchukua uraia wa Kisomalia. Hii ni kwa sababu kesi yake ilihusu swala la ukosefu wa usalama nchi kwao. Fedha zaidi za kununua cheti cha uraia wake mpya zilihitajika. Mtima analipa pauni mia saba (*DY* uk. 120-121).

Ili kuficha ushahidi wa uraia wake halisi, mhamiaji huwa ameshauriwa na wakala wake kuzichanachana stakabadhi zake zote punde tu anapoingia Uingereza (*DY* uk. 79-80). Hata hivyo, mawakala hawawaambii wahamiaji hawa ukweli kuwa pasipoti hiyo inaweza kuwafaa baadaye iwapo watataka kurudi nyumbani.

Mbali na changamoto zinazoambatana na maandalizi ya safari, wahamiaji hukumbwa na changamoto zaidi punde tu wanapofika ughaibuni. Mojawapo ya changamoto hizo ni ukosefu wa kazi. Mhamiaji haruhusiwi kufanya kazi hadi apate kibali cha kufanya kazi, yaani nambari ya bima. Hii huchukua kati ya miezi sita na nane kabla aipate. Mtima alikaa kwa muda wa miezi minane kabla ya kupata namba hiyo. Hata baada ya kuipata nambari ya bima, kazi zenyewe hazipatikani kwa urahisi. Aidha, kazi zinazopatikana huwa duni kama vile kufagia na kuosha vyombo, na malipo yake ni duni (*DY* uk. 119, 120, 123). Waafrika wanaotoka nchi zao wakiwa na matumaini makubwa ya kuyaboresha maisha yao ughaibuni wanaishia kutumikishwa na kufanyishwa kazi duni.

Kutokana na sheria zinazowazuia wahamiaji kufanya kazi kabla ya kupata nambari ya bima, wahamiaji wengi huwa hawana makazi kwa miezi kadhaa baada ya kufika Uingereza. Hii ni kwa sababu wengi huwa hawana pesa za kugharamia kodi. Hivyo basi, hulazimika kuomba makazi kwa wenzao kabla serikali iwaandalie mahali pa kuishi. Mtima, kwa mfano, anamwandikia baba yake baruapepe akimweleza kuhusu ugumu wa maisha yake miezi kadhaa baada ya kuwasili Uingereza. Anamweleza kuwa bado anaishi kwa wenzake ambao tayari wamechoshwa naye. Hata hivyo, hana budi kuvumilia na kung'angania kuishi kwa wenzake hadi apate mahali pake binafsi (*DY* uk. 7).

Changamoto hizi zinamtamausha na kumkatiza tamaa mhamiaji aliyesoma na kuhitimi katika nchi yake. Mtima, kwa mfano, anatamauka kwa sababu alinuia kupata kazi ya heshima na pesa za kumsaidia katika siku zake za baadaye (*DY* uk. 122). Ndoto za wahamiaji za kuboresha maisha yao

zinapofifia wengi wanapata magonjwa mbalimbali. Kwa mfano, Mtima anapata ugonjwa unaogandamiza akili *(depression)*. Analazimika kutumia dawa ili kuupoza (*DY* uk. 124; 153). Hata hivyo, dawa hizo zinamwathiri kwa kumpa usingizi mwingi. Pia zinafanya kichwa na macho yake kuwa mazito. Kwa mtu ambaye ana ugonjwa kama huu bila shaka hataweza kufanya kazi yake vizuri, na hata huenda akaipoteza. Hatimaye ndoto yake ya kuyaboresha maisha ughaibuni inakatika.

Riwaya ya *DY* imedhihirisha kuwa simulizi inayohusiana na maisha bora kwa wahamiaji haiwezi kuaminiwa tena. Hii ni kwa sababu wahamiaji wengi hujipata na changamoto chungu nzima ambazo hawangetarajia kuzipata. Huenda mwandishi wa riwaya ya *DY* analenga kuwazindua na kuwatahadharisha Waafrika kuhusu kufanya maamuzi ya kuhamia nchi za Ulaya bila kutathmini changamoto zinazoambatana na maamuzi hayo.

**Hitimisho**

Uchambuzi wa riwaya za *Dunia Yao* na *Nyuso za Mwanamke* umethibitisha namna S. A. Mohamed ametumia vipengele tofauti vya kibaadausasa kuleta upya katika riwaya ya Kiswahili. Uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mojawapo ya mbinu za kiumbuji alizotumia mwandishi ili kukaidi mtindo wa kimapokeo wa kihalisia. Kila kipande cha simulizi kilisheheni matumizi mengi ya mbinu rejeshi na mbinu elekezi. Ni jukumu la msomaji kuunganisha vipande hivi na kuunda simulizi yenye mantiki. Kimaudhui, matumizi ya vipande vya simulizi ni dhihirisho la hali halisi katika mataifa mengi ya Afrika. Riwaya hizi zimeonyesha kuwa mataifa haya hayana mshikamano kutokana na changamoto yanazozipitia. Imebainika kuwa uongozi mbaya umechangia pakubwa katika kurudisha nyuma maendeleo ya mataifa mengi ya Afrika. Ukoloni mamboleo katika kiwango cha kimataifa umeendelea kudidimiza zaidi mataifa ya Afrika katika umaskini na utegemezi. Riwaya hizi zinawazindua Waafrika watafute njia mbadala za kupambana na changamoto zinazowakumba.

**Marejeleo**


Bakari, M. (2008). *Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za Babu Alipofufuka (2001), Bina_Adam! (2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa Sadiki Ukipenda (2002).* Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).

Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester University Press.

Bertoncini, E. Z. (2009). *Outline of Swahili Literature.* Brill.

Best, S., & Keller, D. (1991). *Postmodern Theory: Critical Interrogations*. Routledge.

Deleuze, G., & Guattari, F. (1984). *Anti-Oedipus*. Kimetafsiriwa na Seem, H. M. & Lane, H. (1984). The Athlone Press.

Hornby, A. S. (2020). *Oxford Advanced Dictionary of Current English*. Oxford University Press.

Khamis, S. A. M. (2003). Fragmentation, Orality and Magic Realism in Kezilahabi's Novel, Nagona. *Nordic Journal of African Studies*. 12(1), 78-91.

Khamis, S. A. M. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novel. *Research in African Literatures* 36(1), 91-108. Indiana University Press.

Khamis, S. A. M. (2008). Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili. Katika: N. O. Ogechi, N. L. Shitemi & K. Simala. *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Moi University Press.

Lewis, B. (2001). 'Postmodernism and Literature'. Katika: Sim S. (mhr) (2001). Routledge

Lyotard, J. F. (1979). *The Postmodern Condition: A Report on Knowledge*. Kimetafsiriwa na Bennington, G. & Massumi, B. (1987). Manchester University Press.

Magaju, J. K. (2004). *Uhalisiajabu katika Riwaya ya Babu Alipofufuka (2001) ya S.A. Mohamed na Bina-Adam! (2002) ya K. W. Wamitila.* Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa).

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mwamzandi, I. Y. (2013). Riwaya za Karne ya 21 na Udurusu wa Nadharia za Fasihi. *Swahili Forum 20 (48-66).*

Ndege, P. O. (2009). *Colonialism and its Legacies in Kenya.* Lecture Delivered during Fulbright – Hay Group Project Abroad Program: July 5th-August 6th, 2009. Moi University.

Rivkin, J., & Ryan, M. (2004). *Literary Theory – An Anthology* (Second Edition). Blackwell Publishing.

Sim, S. (2001). *The Routledge Companion to Postmordernism*. Routledge.

TUKI (2018). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, (Toleo la Nne).* TUKI.

Wamitila, K. W. (2003). Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo*. *Kiswahili* 66, 49-58.

Wamitila, K. W. (2008). *Unaitwa Nani?* Vide-Muwa Publishers.